

'Bajeti ya kilimo inatosha kuleta maendeleo nchini'

Na Lasteck Alfred

KAIMU Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania, Dustan Kaijage ameeleza kuwa bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa ajili ya mwaka wa fedha 2017/18 inatosha kunyanyua sekta ya kilimo nchini.

Akizungumza kwenye mada katika mjadala ulioandaliwa na Taasisi ya Policy Forum iliyohusu 'Kilichobadilika kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi', Kaijage alisema.

Kaijage aliongeza kuwa, bajeti iliyotengwa kwenye wizara hiyo hususani Kilimo si ndogo kama watu wanavyofikiri kwa kuwa kilimo kitanufaika na fedha za wizara nyingine.

"Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwenye bajeti yake ya mwaka huu imeeleza kuhusu uboreshaji wa miundombinu ikiwemo barabara za vijijini. Ukiangalia kwa karibu uboreshaji huo unalenga pia wakulima ili waweze kwenda sokoni kwa unafuu.

"Kuna Wizara ya Maji na Umwagiliaji ambayo nayo imejizatiti kuboresha mifumo na miundombinu ya maji na kufikia watanzania wengi. Je, hapo kilimo hakinufaiki?

Naye Ofisa Uchumi wa Ubalizi wa Denmark nchini, Oscar Mkude alisema Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inapaswa kuweka juhudi kwenye kilimo ili kufikia malengo ya kuwa na Tanzania ya viwanda.

Kwa mwaka wa fedha wa 2017/18, bajeti ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi iliyopitishwa ni Sh bilioni 267.86 ambayo ni sawa na asilimia 0.85 (%) ya bajeti ya mwaka huu ambayo ni Sh trilioni 31.69.

Hata hivyo, wizara hiyo imepanga kutumia Sh bilioni 156.25 kwa ajili ya shughuli za maendeleo wakati Sh bilioni 111.61 itatumika kwenye matumizi.

Bajeti hiyo pia imegawanywa kwa makundi manne ambapo, imetengwa kilimo Sh bilioni 214.81, wakati Mifugo imetengewa Sh bilioni 29.96. Uvuvi nayo imetengewa Sh bilioni 16.79 wakati vyama vya ushirika vimetengewa Sh bilioni 6.29.

Watanzania waalikwa kuisoma vyuo vikuu India